MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

MALALAMIKO NAMBA. GA.71/135/NZ/2021/08

BAINA YA

AYUB ISSA MDETELE ..... MLALAMIKAJI

NA

SHIRIKA LA UGAVI WA UMEME NCHINI (TANESCO).....MLALAMIKIWA

RECEIVED EWURA
10 NOV 2021
NORTHERN ZONE OFFICE

TUZO YA MAKUBALIANO

(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia Waraka wake namba 20 wa tarehe 3 Novemba, 2021)

1.0 Maelezo ya Awali:

Mnamo tarehe 30 Agosti, 2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Ayub Issa Mdetele wa Mtaa wa Viwanda, Kata ya Njoro, Manispaa ya Moshi, mkoa wa Kilimanjaro akilalamikia Shirika la Ugavi wa Umeme Nchini ("TANESCO") ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji amelalamikia makato ya asilimia hamsini (50%) kwenye manunuzi ya umeme wa LUKU ambapo Mlalamikiwa amedai makato hayo ni malipo ya deni la TZS 1,968,585.72 ikiwa ni ankara za matumizi ya umeme ambazo hazikulipwa ("deni bishaniwa").

Mlalamikaji anaeleza kwamba Mlalamikiwa alimjulisha anadaiwa deni la TZS 1,968,585.72 la matumizi ya umeme kwenye dira ya zamani ya malipo baada (*conventional meter*) namba 00032959 yenye jina la Twalibu Mohamed.

Mlalamikaji anaeleza zaidi kwamba Mlalamikiwa amehamishia deni hilo kwenye akaunti ya dira yake ya malipo baada (LUKU) namba 01343122584 na amekua akikatwa asilimia hamsini (50%) kila anaponunua umeme. Mlalamikaji anadai kwamba namba ya dira ya malipo baada (*conventional meter*) aliyokua akitumia ni namba 73036862 na haikua na deni lolote wakati Mlalamikiwa anamuwekea dira ya malipo kabla (LUKU) namba 01343122584. Aidha, Mlalamikaji anadai kwamba alimwandikia barua Mlalamikiwa tarehe 9 Agosti 2021 kuhusu deni analomkata na amefika mara nyingi ofisi za Mlalamikiwa lakini hakuna muafaka uliofikiwa.

Hatimaye, Mlalamikaji alileta malalamiko yake EWURA na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa yafuatayo:

(a) afute deni la TZS 1,968,585.72 na alipeleke kwa mhusika Twalibu Mohamedi;
(b) asitishe makato ya asilimia hamsini (50%) kila anaponunua umeme; na
(c) arudishe kiasi chote cha fedha aliyomkata hadi sasa.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, Mamlaka (EWURA) mnamo tarehe 31 Agosti, 2021 ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa kanuni ya 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 '*Rule 7 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*'.

Mnamo tarehe 30 Septemba 2021, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kuiambia Mamlaka kwamba Mlalamikaji ni mteja wake ambaye kwa sasa anatumia dira ya malipo kabla (LUKU) namba 01343122584. Mlalamikiwa ameeleza kwamba deni la TZS 1,973,585.72 alilowekewa Mlalamikaji limetoka kwenye dira ya malipo baada namba 0002246 kumbukumbu namba 00032959 yenye jina la Twalibu Mohamed. Mlalamikiwa ameendelea kueleza kwamba kwa mujibu wa taarifa za Shirika dira hii ilikua katika nyumba ya Mlalamikaji ambapo deni halisi ni TZS 636,640.67 na riba ni TZS 1,336,945.05. Pia, Mlalamikiwa amefahamisha kwamba baada ya makato kupitia LUKU ya Mlalamikaji kiasi cha deni kilichobaki kwa sasa ni TZS 1,905,585.72.

Mwishoni, Mlalamikiwa amehitimisha kwa kueleza kwakua kumbukumbu za jengo (*Property Reference)* zilikua za Mlalamikaji, Shirika linamshauri kulipa kiasi chote cha deni halisi TZS 636,640.67 ili apatiwe msamaha wa riba ya TZS 1,336,945.05.

Kikao cha usuluhishi baina ya pande zote mbili kilifanyika tarehe 11 na 12 Oktoba 2021 katika Ukumbi wa Hoteli ya Uhuru Mjini Moshi, Kilimanjaro. Katika kikao cha usuluhishi, ilibainika kuwa deni hili linamhusu mtu anyeitwa Twalibu Mohamed ambaye ni jirani yake na Mlalamikaji. Hivyo deni hilo liliwekwa kimakosa kwenye akunti ya Mlalamikaji.

Mwishoni, muafaka kati ya Mlalamikaji na Mlalamikiwa ulifikiwa kwa makubaliano kwamba:

(i) Mlalamikiwa amesitisha makato ya asilimia hamisini (50%) katika dira ya Mlalamikaji kuanzia tarehe 11 Oktoba 2021;
(ii) Mlalamikiwa atafuta mara moja deni la TZS 1,968,585.72 katika dira ya Mlalamikaji namba 01343122584; na
(iii) Mlalamikiwa atamrudishia Mlalamikaji fedha zote alizomkata kupitia manunuzi ya LUKU kiasi cha TZS 78,000. Malipo ya fedha kwa Mlalamikaji yatafanyika kwa njia ya uniti za umeme ndani ya siku kumi na Nne (14) kuanzia tarehe ya makubaliano haya.

Makubaliano haya yamewekwa kwa maandishi kama inavyoainishwa kwenye kanuni ya 14(4) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 '*Rule 14 (4) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*' na kama inavyoanishwa kwenye fomu ya makubaliano.

2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kuwa:

(i) Mlalamikiwa amesitisha makato ya asilimia hamisini (50%) katika dira ya Mlalamikaji kuanzia tarehe 11 Oktoba 2021;

(ii) Mlalamikiwa atafuta mara moja deni la TZS 1,968,585.72 katika dira ya Mlalamikaji namba 01343122584; na

(iii) Mlalamikiwa atamrudishia Mlalamikaji fedha zote alizomkata kupitia manunuzi ya LUKU kiasi cha TZS 78,000. Malipo ya fedha kwa Mlalamikaji yatafanyika kwa njia ya uniti za umeme ndani ya siku kumi na Nne (14) kuanzia tarehe ya makubaliano haya.

Kwa mujibu wa kanuni ya 14(5) ya Kanuni za Taratibu za Kutatua Migogoro T. S. 428/2020 makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila upande utabeba gharama zake katika shauri hili.

IMETOLEWA KWA LAKIRI ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Dodoma tarehe 3 Novemba, 2021.

.....

KAPWETE LEAH JOHN
KATIBU WA BODI